

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**



**MWONGOZO WA UTHAMINI WA FIDIA**

**UMETAYARISHWA NA;**

**KITENGO CHA UTHAMINI**

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

**S.L.P 9132**

**DAR ES SALAAM**

**MACHI 2016**

## **YALIYOMO**

### **Sehemu ya Kwanza:** Utangulizi na Dhana ya Fidia

- 1.0 Utangulizi
- 2.0 Dhana ya Fidia

### **Sehemu ya Pili:** Misingi na Kanuni za Uthamini wa Fidia

- 3.0 Misingi ya Uthamini wa Fidia
- 4.0 Kanuni za Ukadiriaji Fidia

### **Sehemu ya Tatu:** Taratibu za Uthamini wa Fidia

- 5.0 Utaratibu za Maandalizi ya Awali.
- 6.0 Utaratibu wa Uhamasishaji,
- 7.0 Utaratibu wa Ukaguzi wa Mali Uwandani
- 8.0 Utaratibu wa Ukokotoaji Thamani ya Fidia
- 9.0 Utaratibu wa Uandaaji Kitabu cha Majedwali ya Fidia

### **Sehemu ya Nne:** Taratibu za Malipo na Ushughulikiaji Malalamiko ya Fidia.

- 10.0 Taratibu za Malipo ya Fidia
- 11.0 Thamini zenye Malipo ya Ziada
- 12.0 Vyanzo vya Malalamiko na Ushughulikiaji

### **Sehemu ya Tano:** Mambo Mengine ya Kuzingatia

- 13.0 Mambo Mengine ya Kuzingatia katika Uthamini wa Fidia
- 14.0 Wajibu wa Kila Mdau wa Zoezi la Uthamini wa Fidia
- 15.0 Hitimisho

## **VIELELEZO**

- 1) Kielelezo Na. 1: - Nukuu za Vifungu vya Sheria kuhusu Fidia.
- 2) Kielelezo Na. 2: - Nukuu za Vifungu vya Kanuni kuhusu Fidia

- 3) Kielelezo Na 3: - Fomu ya Uelewa Viwango vya Thamani
- 4) Kielelezo Na. 4 - Fomu ya Ukaguzi (VAL FORM 1)
- 5) Kielelezo Na 5: - Fomu ya Ukokotoaji Thamani (VAL. FORM 2)
- 6) Kielelezo Na. 6: - Wajibu wa kila Mdau Kwenye Uthamini wa Fidia
- 7) Kielelezo Na. 7 - Asilimia (%) za Ujenzi (Construction Progress %)

<p><b>SEHEMU YA KWANZA</b></p> <p><b>UTANGULIZI NA DHANA YA FIDIA</b></p>	
<p><b>1.0 UTANGULIZI</b></p>	<p><b>VIELELEZO</b></p>
<p>Swala la fidia katika nchi yetu ni kitu kisichoepukika kulingana na uhitaji mkubwa wa Ardhi kwa miradi yenye manufaa ya umma kama vile kwa ajili ya uwekezaji au shughuli yeyote inayofanywa na Serikali, Taasisi/Mamlaka yeyote ya Serikali au binafsi hasa za maendeleo ya taifa.</p> <p>Mara nyingi na hasa kwa wakati huu ambao Ardhi inatambuliwa ni Mali na Mtaji chini ya Sheria zetu za Ardhi Na. 4 na 5, pamekuwa na ongezeko la mivutano baina ya mamlaka zinazolipa fidia na wananchi wanaolipwa fidia juu ya taratibu za uthamini na viwango halisi vya thamani za mali zao zinazotwaliwa kwa mujibu wa sheria.</p> <p>Kutokana na ukweli kuwa ni haki ya msingi ya mwanachi (ama mfidiwa au mlipaji fidia) kuhoji, kueleweshwa, kulalamika na kusikilizwa kuhusu kupatiwa haki yake ya Fidia; ni dhairi kwamba kuna changamoto nyingi kuhusu maswala ya fidia na hivyo hatuna budi kufuata Misingi na taratibu za uthamini wa Fidia katika hatua zote kikamilifu.</p> <p>Kwa mantiki hiyo mwongozo huu wa utaratibu mzima wa uthamini na ulipaji fidia ni muhimu ili kuweka bayana namna bora zaidi ya uelewa wa pamoja kwa wadau wote wa viwango vya kina (standards) vya kuzingatia na kutumia katika kutekeleza kanuni, taratibu, vigezo na viwango vya misingi ya sheria na taaluma vinavyotakiwa</p>	

<p>kufuatwa.</p> <p>Hivyo, Mwongozo huu unaandaliwa siyo tu kwa ajili ya wataalam wa Uthamini bali kwa manufaa ya wadau wote wenye mahusiano na suala zima la Uthamini na Ulipaji Fidia wakiwemo wafidiwa, walipaji fidia, Mamlaka za Usimamizi na Utoaji haki mbalimbali juu ya ardhi, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali na Binafsi.</p>	
<p><b>2.0 DHANA YA FIDIA</b></p>	
<p>Fidia ni malipo yanayotolewa kwa mtu au Taasisi <b>kama mbadala wa mali yake</b> kutokana na kuondolewa kwenye eneo lake lililotwaliwa kwa manufaa ya umma na kupangiwa matumizi mengine tofauti na yale yaliyopo kwa sasa.</p> <p>Kutwaliwa kwa eneo la mtu kunazingatia Sera na Sheria za Ardhi kuwa ardhi ya Tanzania ni mali ya umma na Rais ndiye mwenye dhamana ya kuulinda kwa manufaa ya wote. Hivyo,</p> <p>Kifungu namba 3 cha Sheria ya Utwaaji (Land Acquisition Act, 1967) kinampa uwezo Mheshimiwa Rais kutwaa Ardhi yoyote pale inapohitajika kwa Manufaa ya Umma.</p> <p>Neno ‘<i>Manufaa ya Umma</i>’ limetafsiriwa katika kifungu Na.4 cha Sheria ya utwaaji kama matumizi ya serikali, miradi ya serikali, kilimo, viwanda, makazi, mahitaji mengine ya jamii..</p> <p>Kutokana na msimamo huo mwananchi anayo haki ya kuitumia na kumiliki kwa muda na masharti yanayoainishwa kwenye hati ya umiliki.</p> <p><b>Hata hivyo</b>, pale ambapo ardhi hiyo inahitajika kutwaliwa kwa ajili ya miradi au shughuli za maendeleo ya taifa zinazofanywa na Serikali, Taasisi/Mamlaka yeyote ya Serikali au Binafsi, Kijiji au mtu basi mmiliki wa asili wa ardhi hiyo; <b>stahili yake ni kulipwa fidia.</b></p> <p>Kifungu Na.11 (i) cha Sheria ya Utwaaji kinaelekeza kuwa pale Ardhi inapotwaliwa serikali inawajibika kulipa fidia. Aidha, Kifungu na. 3(1)(g) cha Sheria ya Ardhi (Sura 113) kinaelekeza kuwa fidia hiyo ni lazima iwe <b>kamilifu, ya haki na ilipwe kwa wakati</b> (<i>fair, full and prompt compensation</i>).</p>	<p><b>Kielelezo Na. 1:</b></p> <p>Nukuu za Vifungu vya Sheria kuhusu Fidia.</p>

<p><b>Mwongozo huu umeandaliwa kwa mujibu wa vifungu namba 3 na 11 vya Sheria ya Utwajaji Na 47, 1967; Kifungu Na.3 (1) (g) cha Sheria ya Ardhi Na. 4 na Na.5 za mwaka 1999; Kanuni za sheria hizi, “The Land (Assessment of the Value of Land for Compensation) Regulation 2001 na kifungu namba 19(1)-(3) cha Kanuni za Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na.5, za mwaka 2001- pamoja na misingi na taratibu za Taaluma ya Uthamini.</b></p>	
--	--

<p><b>SEHEMU YA PILI</b></p> <p><b>MISINGINA KANUNI ZA UTHAMNI NA ULIPAJI FIDIA</b></p>	
<p><b>3.0 MISINGI YA UTHAMINI WA FIDIA</b>  Msingi mkuu wa fidia ya haki, kamilifu na inayolipwa kwa wakati ni kiwango cha thamani ya soko (market value) ya ardhi na maendelezo kwa wakati husika.</p> <ol style="list-style-type: none"> <li>1) <b>Fidia ya Haki (Fair compensation):</b> ni ile inayohakikisha taratibu, vigezo na viwango vya ukadiriaji thamani vyenye usawa baina ya wafidiwa wote na kwa pande zote husika (bila kuegemea au kupendelea/kuonea upande wowote) na yenye uhalisia ya viwango vya soko.</li> <li>2) <b>Fidia Kamilifu (Full compensation):</b> ni ile ya kutosheleza yenye uhalisia wa viwango vya soko kwa wakati uliopo kwa kuzingatia sheria na misingi ya taaluma ya uthamini.</li> <li>3) <b>Fidia inayolipwa kwa wakati (prompt compensation):</b> ni ile inayolipwa ndani ya kipindi cha miezi sita (6) ambayo; <ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kwa mujibu wa Sheria; Kifungu cha 13(2) cha kanuni za sheria ya Ardhi Na.4 za mwaka 2001 na Kifungu cha 19(1)–(3) cha kanuni za Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na.5 za mwaka 2001 ni tangu ardhi ilipotwaliwa au milki kubatilishwa. <b>Lakini,</b></li> <li>➤ Kwa mujibu wa Taaluma ya Uthamini ni tangu taarifa ya uthamini inapoidhinishwa na Ofisi ya Mthamini Mkuu kwa kigezo kuwa hiyo ndiyo tarehe ya thamani hiyo (valuation date/validity).</li> </ul> </li> </ol> <p>Pamoja na kuzingatia bei ya soko, lakini kutokana na kwamba suala la utwaaji linahusisha ‘<i>forced sale</i>’ na siyo suala la ‘<i>willing seller and buyer</i>’ basi sheria imezingatia hilo kwa kulipa fidia inajumuisha posho ambazo ni posho ya upotevu wa makazi, upotevu wa faida, usumbufu, usafiri na gharama za awali katika kupata ardhi.</p> <p>Hivyo, kifungu Na.3(1) (g) cha Sheria ya Ardhi Na.4 ya 1999 na Kanuni zake pamoja na vifungu Na.(7-11) vya kanuni za Sheria ya Ardhi, 2001 zinatuwezeshesha kufikia fidia stahiki</p>	<p><b>Kielelezo Na. 2:</b></p> <p>Nukuu za Vifungu vya Kanuni kuhusu Fidia</p>
<p><b>4.0 KANUNI ZA UKADIRIAJI THAMANI YA FIDIA</b></p>	
<p><b>4.1 Kanuni Kuu ya ukadiriaji Thamani ya Ardhi na Mali Isiyohamishika (Land and Unexhausted Improvements)</b>  Kwa mujibu wa Kifungu Na.3 cha kanuni za Sheria za Ardhi – The Land (Assessment of Value of Land for Compensation Purposes) Regulation, 2001 Kanuni kuu ya ukadiriaji fidia ni thamani ya viwango vya bei ya soko. Hii inajumuisha thamani ya Ardhi, majengo, mazao (mimea na miti) na</p>	

maendelezo mengine kama visma vya maji, makaro, uzio n.k.

#### **4.2 Nani Anayekadiria Thamani ya Fidia**

Kwa mujibu wa vifungu namba 5 na 6 vya kanuni za Sheria ya Ardhi, “*The Land (Assessment of the Value of Land for Compensation) Regulation*”, 2001; uthamini kwa ajili ya fidia unafanywa na Mtaalam wa Uthamini aliyefuzu (Qualified Valuer) na kuhakikiwa/kuidhishwa na Mthamini Mkuu au mwakilishi wake.

#### **4.3 Ni nani Mthamini aliyefuzu (*Qualified Valuer*)**

Kiutaratibu na kiutendaji, ‘*Qualified Valuer*’ ni yule aliyefuzu katika Taaluma ya Uthamini kwenye vyuo vinavyotambulika kitaifa/kimataifa na amejiriwa kama Mthamini kwenye Taasisi inayohusiana na masuala ya Uthamini na kutambuliwa na Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali.

#### **4.4 Njia Kuu za Kitaaluma za Kukadiria Thamani ya Fidia.**

Pamoja na kwamba zipo njia kuu tano (5) zinazotambulika za Uthamini lakini; kwa mujibu wa Kifungu namba 4 cha kanuni za Sheria ya Ardhi, *The Land (Assessment of the Value of Land for Compensation)*, 2001; Thamani ya bei ya soko ya fidia inatakiwa ifikiwe kwa kutumia njia kuu (3) ambazo ni: **Ulinganifu** (*Comparative Method*), **Mapato** (*Income Approach*) and **Gharama** (*Replacement Cost Method*). Hivyo njia inayotumika na misingi ya viwango kwa ardhi, majengo, mazao na posho ni kama ifuatavyo;

- 1) **Ardhi** kwa matumizi mbalimbali kama vile Makazi, Biashara, Makazi/Biashara, Huduma za Jamii, Viwanda n.k; ni ***Comparative Method*** ambapo misingi ya viwango ni bei ya soko kwenye eneo husika katika kipindi cha uthamini.
- 2) **Nyumba/Majengo, Miundombinu** kama vile visima vya maji, visima vya mafuta, makaro na miundo mbinu ya mifano yake ni ***Replacement Cost Method*** ambapo misingi ya viwango ni gharama ya ujenzi toka National Construction Council (NCC) vilivyohuishwa na Mthamini kwa kuzingatia hali halisi ya ujenzi husika (aina/hadhi ya material, workmanship, sifa za mjenzi kama ni Mkandarasi/mwashi na hadhi nyingine kama vile masuala ya mipangomiji.
- 3) **Mazao** ni ***Income Method*** inayozingatia Viwango kwa mujibu wa orodha iliyoandaliwa na kuidhinishwa na ofisi ya Mthamini kwa kushirikiana na mamlaka/taaluma nyingine kama vile za kilimo/misitu na Halmashauri nchini ambavyo misingi yake ni uchambuzi wa takwimu za vigezo vinavyoipa mmea thamani kama vile idadi ya misimu ya uzalishaji, kiwango cha uzalishaji kwenye kila msimu, umri hadi kuanza kuzalisha, umri hadi ukomo wa uzalishaji/kufa, gharama husika, bei ya mlaji shambani n.k.

#### **4) Posho za Kisheria;**

- i. Upotevu wa Makazi unaozingatia viwango vya soko vya kodi ya pango vilivyotafitiwa kwa Nyumba inayojitegemea, Chumba cha Makazi, Chumba cha Biashara, n.k. kwa misingi ya mahali kilipo (mjini/pembeazoni/kijijini n.k)
- ii. Upotevu wa Faida ambayo misingi yake ni kuwepo kwa kumbukumbu za faida yenye uthibitisho wa mkaguzi wa hesabu aliyesajiliwa au mfananisho wa biashara na ushahidi wa ulipaji kodi ya mapato toka Mamlaka ya Mapato Nchini.
- iii. Posho ya Usumbufu ni riba kwa kipindi cha uthamini ambayo misingi ya riba ni wastani wa riba kwenye Benki za Kibiashara katika Akaunti za Amana (Fixed Deposit).
- iv. Posho ya Usafiri ni viwango vya soko vya usafiri wa reli au gari kutokana na takwimu za vyombo vya usafirishaji.
- v. Gharama za kupata ardhi ni uthibitisho wa malipo ya awali (premium, gharama za upimaji kutokana na takwimu za mamlaka husika).

#### **4.5 Ukadiriaji Posho Stahiki**

Posho stahili kwa mfidiwa ni pamoja na posho za upotevu wa makazi, upotevu wa faida, usumbufu na usafiri. Ufafanuzi wa posho hizi ni kama ifuatavyo:-

##### **4.5.1 Posho ya upotevu wa makazi (Accommodation Allowance)**

Posho hii hukadiriwa kwa mujibu wa Kifungu namba 8 cha kanuni za Sheria ya Ardhi, *The Land (Assessment of the Value of Land for Compensation) Regulations*, 2001 ambayo ni gharama ya kukodisha nyumba au chumba kwa mwezi zidisha kwa miezi thelathini na sita (36).

**Angalizo:** Posho hii hulipwa kwenye nyumba iliyokamilika na mfidiwa awe anaishi kwenye nyumba hiyo. Nyumba isiyokamilika hailipwi posho hii.

##### **4.5.2 Posho ya upotevu wa faida(Loss of profit).**

Posho hii hukadiriwa kwa mujibu wa Kifungu Na.9 cha Kanuni za Sheria za Ardhi, 2001 ambayo hukadiriwa vizuri pale vitabu vya hesabu iliyothibitishwa na mkaguzi wa hesabu aliyesajiliwa na Bodi ya Wakaguzi wa Hesabu, zidisha kwa miezi thalathini na sita (36).

**Angalizo:** Posho hii hutolewa kwa biashara inayokutwa ikiendelea wakati ardhi husika ikitwaliwa, na sio biashara iliyopo kwenye mpango wa kuanzishwa. Kodi ya pango la nyumba/vyumba vya makazi au biashara ikiwemo guest house, mahotel n.k. huhesabiwa kwenye **upotevu wa makazi na kamwe siyo upotevu wa faida.**

##### **4.5.3 Posho ya usumbufu (Disturbance allowance)**

Posho hii hukadiriwa kwa mujibu wa kifungu Na.10 cha kanuni za Sheria ya Ardhi ambayo hukadiriwa kwa kuzingatia wastani wa riba inayotozwa katika Benki za Biashara kwa mwaka, kwa



kipindi husika zidisha kwa thamani ya maendelezo ambayo ni:- Thamani ya ardhi + Thamani ya jengo + Thamani ya mimea.

#### **4.5.4 Posho ya usafiri (Transport allowance)**

Posho hii hukadiriwa kwa mujibu wa Kifungu Na.11 cha kanuni za Sheria za Ardhi ambayo ni gharama halisi za usafirishaji (kwa reli au barabara) wa mizigo isiyozidi tani 12 kwa umbali wa kilomita ishirini (20km) kutoka kwenye eneo lililotwaliwa.

**Angalizo:** Posho ya usafiri hailipwi sehemu ambazo hakuna makazi au kuna nyumba haikaliwi au haijakamilika (kifungu namba 12 cha kanuni za Sheria za Ardhi,2001).

#### **4.5.5 Gharama za awali za kupata Ardhi (Cost of acquiring subject land).**

Kifungu Na.3 (1) (g) (v) cha Sheria za Ardhi Na4, 1999. Hizi ni gharama zinazoweza kuthibitishwa kama vile malipo ya awali (Premium) na gharama za upimaji (survey costs). Gharama za upimaji zinazolipwa zinatakiwa ziwe ni zile zinazoendana na hali halisi ya upimaji wakati wa utwaaji wa eneo hilo.

<p><b>SEHEMU YA TATU</b></p> <p><b>TARATIBU ZA UTHAMINI WA FIDIA.</b></p>	
<p><b>5.0 UTARATIBU WA MAANDALIZI YA AWALI</b></p>	
<p><b>5.1 Maandalizi ya awali (<i>pre-site inspection</i>).</b></p> <ol style="list-style-type: none"> <li>1) Kupokea na kutafakari Maelekezo (Instructions) yanayoainisha ukubwa wa eneo (ramani), kiwango cha uendelezaji na uthibitisho wa uwepo wa fedha ya kulipa fidia kwa wakati.</li> <li>2) Kutembelea eneo husika (baada ya kumtaarifu au kumshirikisha Mthamini wa Halmashauri husika) akiambatana na viongozi wa hilo eneo/mradi husika na wataalam muhimu.</li> <li>3) Kufanya maandalizi ya viwango vya thamani ya ardhi, majengo na posho za kisheria.</li> <li>4) Kufanya mawasiliano na ofisi ya Kamishna wa Ardhi/ Afisa Ardhi Mteule kwa ajili ya maandalizi ya Land Form No.69.</li> <li>5) Kufanya maandalizi ya vitendea kazi kama vile rangi, vibao, camera/betri, shajara, Val Form 1 &amp; 2, n.k.</li> <li>6) Kutoa Namba ya Kumbukumbu ya Uthamini (VAL/No.).</li> <li>7) Kutoa mafunzo ya uelewa wa pamoja kwa timu za watendaji.</li> <li>8) Kushiriki kwenye vikao vya kuhamasisha na kutoa elimu kuhusu mradi kwa wananchi wanaoathirika.</li> <li>9) Kufungua file kwa ajili ya kumbukumbu za zoezi husika kuanzia barua ya maelekezo (instructions), mihutasari ya vikao vya mradi ikiwemo vikao vya uhamasishaji, fomu ya uelewa wa viwango vya thamani vitakavyotumika, nakala ya taarifa ya uthamini, barua za malalamiko na ushughulikiaji wake, n.k.</li> </ol>	
<p><b>5.2 Maandalizi ya Viwango vya Uthamini</b></p> <ol style="list-style-type: none"> <li>1) Maandalizi ya awali ni pamoja na viwango vya uthamini wa mali (ardhi, nyumba/majengo, mazao, posho mbalimbali za kisheria na riba) ambavyo wananchi wahusika watataarifiwa kwenye vikao vya uhamasishaji.</li> <li>2) Hivyo Mthamini Kiongozi (kiongozi wa zoezi zima la uthamini husika); atafanya utafiti katika eneo husika ili kubaini bei za soko na kisha kufanya uchambuzi wa kina wa viwango stahiki vya thamani ya mali.</li> <li>3) Kutokana na utafiti na uchambuzi huo, Mthamini Kiongozi kwa kuwasiliana na Mthamini wa Halmashauri husika (Mthamini Mkazi – Resident Valuer) atajaza viwango hivyo kwenye Fomu ya ‘Uelewa wa Viwango (<b>Kielelezo Na. 3</b>).</li> <li>4) Kisha Fomu hiyo kupitia kwa Mthamini wa Halmashauri husika itawasilisha mapendekezo ya viwango kwenye Ofisi ya Mthamini Mkuu au ya Kanda husika kwa ajili ya kuhuishwa na kupata ridhaa ya kutumika.</li> <li>5) Aidha, katika kuwezesha mikutano ya uhamasishaji, nakala ya fomu ya viwango itatolewa kwa wananchi, Mkuu wa Wilaya na Mamlaka/Wadau wengine kadri itakavyoonekana inafaa pamoja na kubandikwa kwenye Ofisi za Kata na Serikali za Mitaa husika.</li> </ol>	<p><b>Kielelezo Na 3:</b></p> <p>Fomu ya Uelewa Viwango vya Thamani</p>

<p><b>6.0 UTARATIBU WA UHAMASISHAJI</b></p>	
<p><b>6.1 Uhamasishaji Mradi</b></p> <ol style="list-style-type: none"> <li>1) Zoezi la uthamini wa mali za wananchi ni lazima litanguliwe na mikutano ya kutoa elimu na kuhamasisha wananchi na viongozi wa eneo husika juu ya mradi husika sambamba na zoezi husika la uthamini kwa ajili ya stahili ya fidia.</li> <li>2) Hatua hii ni muhimu katika zoezi la uthamini ili kuhakikisha uwazi na ushirikishwaji wa wananchi na viongozi kwenye zoezi hili.</li> <li>3) Mikutano ya uhamasishaji iongozwe na Mkuu wa Wilaya/Mwakilishi wake pamoja na viongozi wengine wa Wilaya, Halmashauri ya Wilaya, Ofisi ya Mwekezaji au mlipaji fidia na wataalam husika wa sekta ya ardhi.</li> <li>4) Katika vikao vya uhamasishaji viongozi wa wilaya, mamlaka ya ulipaji fidia, wataalamu wa Sekta ya Ardhi na wengine kadri itakavyoonekana inafaa washiriki na wawafahamishe wananchi faida ya mradi na taratibu za kisheria na stahili zao.</li> <li>5) Katika vikao hivyo wataalam wawajibike kutoa ufafanuzi wa hoja za wananchi kuhusiana na maeneo ya taaluma zao kama yalivyoainishwa kwenye Kielelezo Na. 11 cha Wajibu wa kila Mdau Kwenye Uthamini wa Fidia.</li> <li>6) Aidha, Mihtasari ya vikao vya uhamasishaji iandaliwe vizuri na isainiwe kwa mujibu wa taratibu zilizopo. Mihtasari hii iorodheshe majina ya wajumbe walioudhuria na saini zao.</li> </ol>	
<p><b>6.2 Uhamasishaji Zoezi la Uthamini</b></p> <p>Katika vikao hivyo vya uhamasishaji; <b>Mthamini</b> kama muhusika mkuu, atawajibika kueleza kwa ufasaha masuala yafuatayo;</p> <ol style="list-style-type: none"> <li>1) Taratibu za uthamini na ulipaji fidia ikiwemo utaratibu wa ukaguaji mali za wananchi, upimaji ardhi na majengo,</li> <li>2) Utaratibu wa kuhesabu mimea kwa kuweka wazi ni katika mazingira gani na kwa mimea ipi Mthamini atahesabu mmea mmoja mmoja au ‘cluster’ kwa maana ya shina au ukubwa wa eneo.</li> <li>3) Utaratibu utakaotumika katika kuhesabu mimea pale <b>penye tatizo la upandaji au ujenzi holela unaozidi kiwango (overcropping/development)</b> ikiwemo kutotambua mazao au nyumba zilizoendelezwa wakati zoezi linaanza.</li> <li>4) Viwango vya soko vya thamani ya mali (ardhi, majengo, mazao na posho stahiki) vitakavyotumika kwenye uthamini husika.</li> <li>5) Utaratibu wa kuhesabu muda stahiki wa kutoza riba ya ucheleweshaji na kiwango cha riba cha kutozwa.</li> <li>6) Wananchi waelezwe umuhimu wa kuwa makini wakati wa zoezi la kuhesabu mali, na kuwa wathibishe hilo kwa kusaini Val Form 1, ambapo nakala moja ataachiwa mfidiwa baada ya kusainiwa na kiongozi wa eneo.</li> <li>7) Wananchi waelezwe haki yao ya kuona jedwali la mahesabu ya fidia yao kabla ya kuchukua fidia.</li> <li>8) Kuweka wazi muda wa ukomo wa kuwasilisha malalamiko ya fidia.</li> <li>9) Wananchi waelekezwe mfumo/mahali pa kuwasilisha malalamiko yao kwa wakati.</li> <li>10) Ikibidi mthamini aweke wazi suala la uwepo wa asilimia za uchakavu ili kuondoa hoja nyingi kutoka kwa wananchi kuhusiana na viwango pungufu kwa mitamraba wanavyopewa tofauti na vile walivyotangaziwa wakati wa uhamasishaji.</li> </ol>	
<p><b>7.0 UTARATIBU WA UKAGUZI WA MALI UWANDANI</b></p>	

<p><b>7.1 Ukaguzi wa Mali Uwandani (Site Inspections)</b></p> <ol style="list-style-type: none"> <li>1) Ukaguzi wa mali hufanywa na timu inayoshirikisha <i>Mthamini, Mpima (adjucator), mfidiwa/mwakilishi wake, Mjumbe wa Serikali ya Mtaa/eneo husika</i>) na <i>Mlipaji fidia/mwakilishi wake</i></li> <li>2) Taarifa za ukaguzi ziandikwe kwenye fomu ya ukaguzi (VAL. FORM 1) <b>Kielelezo Na. 4</b></li> <li>3) Mthamini ndiye mwandishi wa taarifa za ukaguzi ambaye atawajibika kujaza Val. Form 1.</li> <li>4) Taarifa hizo za ukaguzi zitamkwe kwa uwazi kabla Mthamini hajazijaza kwenye fomu ya ukaguzi hasa taarifa kuhusiana na vipimo au idadi ya mali.</li> <li>5) Fomu ya ukaguzi ijazwe kikamilifu kuonyesha maelezo ya mali zote ikiwemo vipimo, michoro, aina na idadi za mali n.k. kwani taarifa hizi ndizo zitamwezesha Mthamini kuamua kiwango kwa mitamraba (Rate per square meter) cha kutumia.</li> <li>6) Ukaguzi uanze kwa kubaini mipaka ya <b>kipande cha ardhi/shamba</b> la mfidiwa (Adjudication) sambamba na Mpima (adjudicator) kuchukua vipimo vya ardhi/shamba kwa kutumia vifaa vya kisasa vya upimaji. <b>Angalizo:</b> Kamwe, adjudication isifanyike kwa kutumia futikamba au hatua za miguu.</li> <li>7) Aidha, <b>ukaguzi wa mazao</b> ufanyike kwa kuhesabu idadi ya kila aina ya zao lililopo na kiwango cha ukuaji. Hata hivyo suala la kiwango cha ukuaji ni suala la utashi wa mtaalam wa uthamini. <b>Angalizo:</b> Endapo Mthamini atabaini uwepo wa upandaji wa hila wa mazao (overcrpping); busara na standards za taaluma ya Kilimo zitumike kuhesabu hayo mazao.</li> <li>8) Kisha <b>ukaguzi wa nyumba</b> unaobainisha idadi na hadhi ya majengo yaliyopo kama vile nyumba kubwa na nyumba za uani, gorofa au single storey nk, taarifa za aina ya ujenzi, vifaa vilivyoyumika kuanzia paa, ukuta, madirisha, milango, sakafu na finishes bila kusahau huduma zilizopo kama vile maji na umeme, idadi ya vyumba na matumizi ya kila chumba.</li> <li>9) Aidha, vipimo vya nyumba vichukuliwe kwa kutamka kwa uwazi vipimo hivyo kwa ajili ya timu kuviifiki kabla Mthamini hajajaza kwenye mchoro kwenye fomu ya ukaguzi.</li> <li>10) Kisha miliki apigwe picha akiwa ameshikilia bango lenye namba ya uthamini (Val/No.) akiwa mbele /kwenye eneo la mali zake.</li> <li>11) Mwisho Fomu za ukaguzi zisainiwe na mwenye mali, kiongozi wake wa serikali ya Mtaa au Mwakilishi/Mjumbe na Mthamini kwa kushuhudiwa na washiriki wengine kama vile mwakilishi wa mlipa fidia kadri itakavyoonekana.</li> <li>12) Mfidiwa apatiwa nakala ya hiyo fomu ya ukaguzi iliyojazwa na kusainiwa kikamilifu.</li> <li>13) Baada ya ukaguzi alama za kudumu ziwekwe katika mali iliyokaguliwa/thaminiwa.</li> </ol> <p><b>Angalizo:</b> Timu ya ukaguzi inawajibika kuzingatia yanayobainishwa ana kwa ana kwenye ukaguzi na hatimaye taarifa hiyo ndiyo itakayotumiwa na Mthamini katika kukokotoa fidia stahiki. Hivyo timu ya ukaguzi na Mthamini haifungwi na lolote nje ya taarifa hiyo ikiwemo Land Form 70 bali yanayojiri au kubainishwa kwa uwazi siku na saa ya ukaguzi.</p>	<p><b>Kielelezo Na. 4:</b></p> <p>Fomu ya Ukaguzi (VAL FORM 1)</p>
<p><b>7.2 Mfumo wa Kuhesabu Mazao (Idadi na Kiwango cha Ukuaji)</b></p> <p><b>1) Maelezo ya Jumla</b></p> <p>Katika kuhesabu mazao ya wafidiwa, ni vizuri Mthamini kutambua aina ya mfumo wa kuhesabu mali unaozingatia hali halisi ya upandaji/uotaji wa mazao ya aina mbalimbali; na wananchi</p>	<p><b>Kielelezo Na. 5.</b></p> <p>Ujazo/Idadi ya Mazo/Miti kwenye eneo la Hekta, Ekari, na</p>

<p>wakataarifiwa aina ya mifumo yote itakayotumika kulingana na aina ya mazao &amp; hali ya upandaji.</p> <p>Aidha ieleweke kuwa, kwa mujibu wa Taaluma ya Kilimo, ipo <i>schedule</i> inayoanisha kiwango cha juu cha Ujazo/idadi ya mazao kwa Hekta ambacho kutokana na taaluma hiyo imezingatia mahitaji ya nafasi kati ya mmea na mmea (<b>Kielelezo Na. 5</b>).</p> <p>Hivyo, hasa kwa mazao ya kudumu, fidia iliyoonyeshwa kwa kila mitamraba au hekta moja ni kiwango cha juu kabisa ambacho mkulima anaweza kulipwa kwa eneo hata kama idadi ya mimea iliyomo kwenye shamba lake inazidi ile iliyoonyeshwa kwa zao linalohusika.</p> <p>Vigezo vya ujazo kwa mita za mraba kwa mimea vinazingatia tabia ya mmea kujitawanya (canopy cover), asilimia ya ukuaji na utapakaaji wa mizizi.</p> <p>Utafiti umedhihirisha kuwa mti wa kudumu katika kiwango cha asilimia 100, unahitaji eneo la mita 22 za mraba sawa na wastani wa miti 178 kwa ekari</p> <p>Kwa mantiki hiyo, ni muhimu kila Mthamini akajua idadi ya ujazo kwa kila mmea kwa hekta na nafasi inayotakiwa kuzingatiwa kati ya mmea na mmea ili kuweka idadi sahihi ya mimea katika shamba wakati wa uthamini.</p> <p>Iwapo itatokea Mthamni atakutana na hali ambayo idadi ya mazao katika ekari/hekta ya mraba ni kubwa kuliko inavyokubalika na miongozo ya kilimo. Mthamini anaelekezwa kuhesabu kwa kuzingatia idadi ilivyoelekezwa kwenye miongozo ya kilimo na si vinginevyo.</p> <p><b>2) Mfumo wa Kuhesabu idadi ya Mazao</b> Ipo mifumo tofauti ya kuhesabu mazao ambayo inatokana na uwepo wa mimea kama ifuatavyo:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Inayota mmoja moja na kujulikana kama <b>mimea/miti</b>.</li> <li>• Inayoota kwa pamoja/mafungu yanayotokana na machipukizi yake na kujulikana kama <b>shina moja</b>.</li> <li>• Inayoota kwa kujisambaza kwenye eneo la ardhi na siyo rahisi kuhesabu mmoja mmoja au shina bali kwa kipimo cha ukubwa wa eneo au tuta inayokalia.</li> </ul>	<p>Mitamraba.</p>
--	-------------------

<p><b>Hivyo mifumo ifuatayo ni vema ikazingatiwa katika kuhesabu mazao.</b></p> <ol style="list-style-type: none"> <li>i. Mfumo wa kuhesabu mimea mmoja mmoja (<b>head counting</b>) mfano ni miti ya kudumu kama vile miti ya matunda, mazao ya biashara na miti ya mbao n.k,</li> <li>ii. Mfumo wa kuhesabu kwa mafungu/shina (<b>cluster counting</b>) mfano ni migomba, magimbi, miwa, katani. <ul style="list-style-type: none"> <li>• Mimea hii hunza kutoa mashina/chipulizi katika kiwango cha ukuaji cha asilimia 80 na kuendelea.Hivyo, uhesabu wa mafungu unajumuisha mti mkubwa na machipukizi yake kuwa shina moja</li> <li>• Aidha, katika hili, pale ambapo mimea hii imetawanywa, mimea (3) huhesabiwa kama shina moja.</li> </ul> </li> <li>iii. Mfumo wa kuhesabu kwa ukubwa wa eneo (<b>area counting</b>) kwa mitamraba, ekari hekta au tuta mfano ni mazao ya msimu kama vile kunde, mbogamboga, baadhi ya nafaka.</li> <li>iv. Hivyo,inassitizwa kuwa, yale mazao yanayotakiwa kuhesabiwa kama ekari au shina yahesabiwa hivyo, na wananchi waelezwe utaratibu huo kabla ya zoezi kuanza.</li> </ol> <p>Eneo lenye mazao mchanganyiko (<i>intercropped</i>) ya kudumu na ya msimu ndani ya shamba moja. Kwa Mazao ya kudumu hesabu itachukuliwa kwa kuhesabu mti mmoja mmoja, wakati mazao ya msimu hesabu itachukuliwa kwa kupima ukubwa wa eneo la mraba lenye mazao ya msimu.</p>	
<p><b>8.0 UTARATIBU WA UKOKOTOAJI THAMANI YA FIDIA</b></p>	
<p><b>8.1 Ukokotoaji wa thamani:</b></p> <ol style="list-style-type: none"> <li>1) Taarifa za uwandani zilizoko kwenye fomu ya ukaguzi (Val. Form 1) zihamishiwe kwenye form ya ukokotoaji (Val.Form 2).</li> <li>2) Ukokotoaji wa thamani ufanyike kwa mujibu wa <b>viwango vya soko</b> vilivyotafitiwa katika eneo husika na kuridhiwa na Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali.</li> <li>3) Ni jukumu la kila mthamini kuhakikisha kuwa viwango vya thamani anavyotumia vinaenda na bei ya soko kwa wakati huo kwenye eneo husika la uthamini.</li> <li>4) Aidha, Mthamini anahitajika kuwa mweledi katika kutambua viwango sahihi vya ukuaji wa mazao; asilimia za uchakavu (depreciation) na ukamilivu wa ujenzi (% of progress) kwa Majengo.</li> <li>5) Baada ya ukokotoaji wa thamani ya fidia; fomu zote za ukaguzi na mahesabu ziwasilishwe kwa Mthamini Kiongozi kwa ajili ya kukaguliwa na kuthibitishwa.</li> <li>6) Kisha taarifa ya uthamini ambayo pia ni sehemu ya kitabu cha majedwali ya fidia iandaliwe.</li> </ol>	<p><b>Kielelezo Na 6:</b></p> <p>Fomu ya Ukokotoaji Thamani (VAL. FORM 2)</p>
<p><b>8.2 Uwekaji Aslimia (%) za ukuaji katika Uthamini wa Mazao</b></p> <p>Mthamini ajitahidi kuwa mwangalifu katika uwekaji asilimia, kwa kuhakikisha asilimia ya ukuaji inayowekwa inawiana na ukubwa wa mimea. Asilimia kuu za ukuaji ni kama ifuatavyo.</p> <ol style="list-style-type: none"> <li>i. Mimea/Miti inayozalisha ===== 100%</li> <li>ii. Mimea/Miti iliyopevuka ===== 60%</li> <li>iii. Mimea/Miti michanga ===== 30%</li> <li>iv. Mimea/Miti Mikongwe ===== 50%</li> </ol>	

<ul style="list-style-type: none"> <li>● Fidia iliyoonyeshwa kwa mazao ya kudumu italipwa kwa asilimia 100 kwa mazao yanayozalisha kwa kiwango cha juu</li> <li>● Fidia itakuwa asilimia 60 ya viwango hivyo iwapo mimea itakuwa imepevuka kiasi cha kuanza kuzaa (au imetimiza miaka 3 tangu kupandwa) lakini bado kufikia kutoa mavuno ya wastani.</li> <li>● Kwa mimea ambayo bado kuzaa, fidia itakuwa asilimia 30 ya viwango vilivyoonyeshwa.</li> <li>● Fidia kwa miche iliyo kitaluni itakuwa asimila 10 iwapo haitawezekana kuihamisha.</li> <li>● Mimea ambayo itakuwa mikongwe na haitoi mazao itakuwa na fidia ya asilimia 50 ya viwango.</li> </ul> <p><b>Viwango kwa asilimia kwa mazao itategemea sana umri na matunzo ya mazao husika. (Miaka mitatu - uzao wa kwanza, miaka mitano – uzao wa kati na miaka 8 na kuendelea – uzao wa kutosheleza).</b></p>	
<p><b>8.3 Uwekaji asilimia (%) ya Uchakavu (Depreciation %)</b>  Katika kufanya uthamini ni lazima kiwango cha uchakavu (Depreciation) kitolewe kulingana na dosari/kasoro zilizobainishwa na kuorodheshwa wakati wa ukaguzi ili kutoa uthibitisho (justification) wa asilimia iliyotumika katika ukokotozi wa thamani ya fidia.</p> <p>Katika Uthamini wa Fidia tutahusika zaidi na uchakavu wa dosari za mwonekano (physical Obsolescence) kuliko zile za <i>Economic, Functional</i> na <i>technological obsolescence</i>.</p> <p>Katika kuweka viwango vya asilimia ya uchakavu, Mthamini atumie weledi wake na Mwongozo wa Viwango vya Majengo ili kuweka asilimia stahiki.</p>	
<p><b>8.4 Uwekaji Asilimia (%) za Ukamilivu wa Ujenzi (% of Construction Progress)</b>  Katika kuonyesha asilimia ya ujenzi kwa majengo ambayo hayajakamilika kitabu cha Wood (1964) “Valuation Handbook” kitumike ili kuonyesha asilimia ya ujenzi iliyofikiwa (percentage of progress). Kwa urahisi wa rejea nakala ya kurasa husika imeambatishwa kama <b>Kielelezo Na. 7</b></p>	<p><b>Kielelezo Na. 6</b>  Asilimia (%) za Ujenzi (Construction Progress %)</p>
<p><b>9.0 UTARATIBU WA UANDAAJI KITABU CHA MAJEDWALI YA FIDIA</b></p>	
<p><b>9.1 Utayarishaji Vitabu vyaHati/Majedwali ya Fidia na Kuidhinishwa:</b>  Majedwali ya fidia hutayarishwa kwa kuzingatia taarifa iliyopo kwenye fomu ya ukokotoaji (Val. Form 2). Hivyo, Mthamini atatengeneza nakala sita (6) za kitabu cha Jedwali la fidia (<i>Compensation Schedule - VAL. FORM 3</i>) kwa <i>format</i> yoyote ila ni lazima iwe na mpangilio wa sehemu kuu nne (4) zifuatazo;</p>	

- 1) **PART I: - Introductory Notes (Utangulizi)**
- 2) **PART II: - Valuation Summary (Muhtasari wa Fidia)**
- 3) **PART III: - Detailed Compensation Schedules (Hati za Fidia).**
- 4) **PART IV: - Attachments (Viambatisho)**

Maelezo ya kina ya maudhui ya kila sehemu ni kama ifuatavyo.

**1) PART I: - Introductory Notes (Utangulizi)**

Sehemu ya Utangulizi kama ilivyo kwenye taaluma ya uthamini ni lazima ionyeshe;

- i. Instruction and purpose of valuation (maelekezo na madhumuni ya uthamini).
- ii. Scope of the work: Lands (acres)/ buildings or structures/ cops and trees.(Ukubwa wa kazi kuwa unahusisha mali gani na eneo/coverage ya kiasi gani)
- iii. Methods and basis of valuation (njia ya uthamini iliyotumika na msingi wa viwango vya thamani).
- iv. **Angalizo:**- taja ile njia au msingi tu uliotumika kwenye uthamini husika na siyo kutaja nadharia zote unazozijua kuhusinana na njia au msingi unazozifahamu. Mfano taarifa ni lazima itamke wazi kuwa , **msingi (Basis)** iliyotumika ni ipi kati ya zifuatazo;
  - *Market Value* kwa thamani ya ardhi,
  - *Depreciated Replacement Cost* kwa thamani ya majengo na
  - *Crop Compensation Schedule* kwa thamani ya mazao

Aidha **njia (method)** za uthamini zilizotumika ni zipi kati ya zifuatazo;

- Comperative method kwa thamani ya ardhi,
- Replacement Cost kwa thamani ya majengo
- Income Method katika kuunda Crop Compensation Schedule.

Pia taarifa lazima iweke wazi kuhusu vyanzo vya viwango vya posho vilivyotumika kama vile mamlaka ya usafiri (posho ya usafirishaji), aslimia ya riba (posho ya usumbufu).

- v. Confidentiality clause.
- vi. **Validity clause:** muda wa utahmini kisheria ambapo baada ya miezi sita (6) tangu ilipoidhinishwa na Ofsis ya Mthamini Mkuu, kutakuwa na tozo la riba.
- vii. **Third part information liability:** maelezo ambayo mthamini amelazimika kuyaamini na kuyatumia katika uthamini wake lakini hawajibiki nayo (not liable).
- viii. **Date of inspection and valuation:** Tarehe ya ukaguzi na uthamini
- ix. **Valuation reporting and summary:**  
Part I: Introductory Notes.

Part II: Valuation summary (Muhutasari wa fidia).



Part III: Detailed Compensation Schedules (Hati za Fidia).

Part IV: Attachments; - Orthophoto map or Polygons of Respective area.

- x. **Opinion of Value** (thamani ya ujumla ya fidia kwa tarakimu na maneno).
- xi. **Certification:** (Saini na Muhuri wa Mthamini/ Mthamini Kiongozi husika)
- xii. **Approval:** (Saini na muhuri wa ofisi ya Mthamini Mkuu).

**2) PART II: - Valuation Summary (Muhtasari wa Fidia)**

Sehemu ya muhtasari iwasilishe orodha ya wafidiwa na thamani ya fidia kwa mpangilio rahisi wa rejea ama kwa ‘*alphabetical order*’ ya majina (A-Z) au Namba za Uthamini (val nos.1 – 100 na kuendelea). Aidha iwe na column zenye vichwa vya taarifa zifuatazo kwenye kila ukrasa;

- i. Namba ya kumbukumbu (Serial No.).
- ii. Namba ya Uthamini (Val. No.)
- iii. Jina la Mfidiwa husika.
- iv. Jumla ya thamani ya Fidia anayostahili kulipwa.
- v. Sehemu ya Picha na saini ya Mfidiwa wakati wa malipo.
- vi. Kila mwisho wa kila ukurasa uwe na sehemu za saini za Mthamini Kiongozi, Mthamini Mkuu, Afisa Ardhi Mteule, Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa na Mhasibu Mlipaji. Pale inapobidi mathalan kutokana na wingi wa kurasa za Muhtasari, basi saini ya Mkuu wa Wilaya na Mkoa iwepo kwenye ukurasa wa mwisho tuu wa sehemu ya Muhtasari.

**3) PART III: - Detailed Compensation Schedules (Hati za Fidia).**

Sehemu hii inawasilisha mchanganuo/hesabu kwa kina ambao utaonyesha hesabu ya kila aina ya mali (ardhi, nyumba na mazao) pamoja na posho anayostahili kila mwananchi ikionyesha

- i. Namba ya kumbukumbu (Serial No.).
- ii. Namba ya Uthamini (Val. No.)
- iii. Picha ya Mfidiwa
- iv. Jina/majina kamili ya Mfidiwa husika.
- v. Mahali/eneo lilipo
- vi. Maelezo ya mali, jengo/mmea
- vii. Kiwango cha thamani ya Ardhi
- viii. Ukubwa wa Ardhi
- ix. Idadi na kiwango cha thamani kwa kila zao
- x. Kiwango cha ukuaji wa kila zao kwa asilimia (%)
- xi. Gharama ambazo mlipwaji fidia aatakuwa alikutana nazo wakati wa uendelezaji Ardhi kama vile visima, uwekaji wa umeme na maji, urekebishwaji wa alama za mpaka, mashimo ya choo, uhamishwaji wa vifaa/mashine nzito kwa kutumia mashine nzito (crane) n.k.
- xii. Thamani halisi ya mali (majengo, mazao, ardhi, posho n.k.)

**5) PART IV: - Attachments (Viambatisho)**

<p>Viambatisho muhimu ni pamoja na;</p> <ol style="list-style-type: none"> <li>i. Barua/Nyaraka ya ombi/maelekezo ya uthamini</li> <li>ii. Ramani ya eneo la kazi na umiliki wa wafidiwa</li> <li>iii. Ramani ya picha za anga (Orthophoto map) yenye kuainisha vipande vya ardhi (Polygons) za kila mfiwa.</li> <li>iv. Nakala ya fomu ya uelewa wa viwango vya uthamini huo</li> <li>v. Schedule ya viwango vya mazao.</li> <li>vi. Fomu ya uthibitisho kuwa ukaguzi/uthamini ulikuwa shirikishi, wazi na ulizingatia taratibu zote za uwandani na taaluma</li> </ol>	
<p style="text-align: center;"><b>9.2 Kusainiwa-Hati/Majedwali ya Fidia.</b></p> <p>Kwa mujibu wa kanuni za Sheria ya Ardhi, 2001. Uthamini wa mali kwa ajili ya fidia ni lazima uhakikiwe na kusainiwa na Mthamini Mkuu au wakilishi wake. Aidha Kwa mujibu wa utaratibu wa kiutawala, majedwali ya Fidia kusainiwa katika ngazi za Halmashauri, Wilaya na Mkoa Husika.</p> <p>Hivyo baada ya kukamilika kwa utayarishaji wa nakala sita (6) za kitabu cha majedwali na kusainiwa na Mthamini Kiongozi; huwasilishwa kwa Mthamini Mkuu na kisha kwa viongozi wanapaswa kusaini kama ifuatavyo;</p> <ol style="list-style-type: none"> <li>1) <b>Mthamini Kiongozi</b>; ambaye baada ya kuandaa kitabu ataweka muhuri na kusaini ukurasa unaoonyesha thamani nzima ya fidia (opinion of Value) ambayo ni ukurasa wa mwisho wa Sehemu ya Kwanza ya kitabu (Utangulizi) kisha atawasilisha vitabu hivyo kwenye ofisi ya Mthamini Mkuu. Jedwali la fidia litakalo tambulika ni lile lililo idhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali.</li> <li>2) <b>Mthamini Mkuu/Mwakilishi wake</b>; baada ya kuhakiki ataidhinisha taarifa ya uthamini kwa kuweka muhuri na saina ukurasa wa mwisho wa Sehemu ya Kwanza na pia kurasa zote za Sehemu ya Pili (Muhtasari).</li> <li>3) <b>Aidha</b>, katika ngazi nyingine watasaini kwenye kurasa zote za Sehemu ya Pili (Muhtasari) au pale inapobidi watasaini ukurasa wa mwisho tu wa Sehemu hiyo ya Muhtasari. Ngazi hizo ni; <ol style="list-style-type: none"> <li>i. Afisa Ardhi Mteule wa Halmashauri ya eneo husika;</li> <li>ii. Mkuu wa Wilaya (DC) wa Wilaya ya eneo husika.</li> <li>iii. Mkuu wa Mkoa (RC) wa Mkoa wa eneo husika.</li> <li>iv. Mhasibu Mlipaji</li> </ol> </li> </ol> <p>Baada ya taratibu za maandalizi ya kitabu cha majedwali ya fidia kukamilika na kusainiwa, nakala za vitabu zisambazwe kama ifuatavyo;</p> <ol style="list-style-type: none"> <li>1) Nakala mbili (2) kwa Mlipa fidia</li> <li>2) Nakala moja moja (1) kwa Ofisi za Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Mthamini Mkuu wa Serikali na Mthamini Kiongozi.</li> </ol>	

<p><b>SEHEMU YA NNE</b></p> <p><b>TARATIBU ZA MALIPO NA KUSHUGHULIKIAJI MALALAMIKO YA FIDIA</b></p>	
<p><b>10.0 TARATIBU ZA MALIPO YA FIDIA</b></p>	
<p><b>10.1 Aina za Malipo ya Fidia</b> Kwa mujibu wa Kifungu na. 10 ya Kanuni ya sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999, “The Land (Compensation Claims) Regulations, 2001; aina za malipo ya fidia ni kama ifuatavyo;</p> <ol style="list-style-type: none"> <li>1) <b>Fedha tasilim</b> - ambayo kiutendaji yaweza kuwa tasilim au kwa mfumo wa Hundi.</li> <li>2) <b>Ardhi</b> - yenye ukubwa na ubora/hadhi sawa na ile iliyotwaliwa.</li> <li>3) <b>Jengo</b> - lenye ukubwa na ubora/hadhi sawa na lile lililotwaliwa.</li> <li>4) <b>Mimea/miti ya mazao</b> (Plants &amp; seedlings).</li> <li>5) Haki au ruhusa ya <b>kutumia mali ya jamii</b> kwa muda maalum (Access to communal Assets) mf. Maji, malisho, n.k</li> <li>6) Utoaji wa <b>nafaka na vyakula vingine</b> kwa muda maalum (Regular supplies of grain &amp; other basic food staffs for specified time).</li> <li>7) <b>Aina nyingine yeyote</b> kwa mujibu wa makubaliano.</li> </ol>	
<p><b>10.2 Ulipaji Malipo ya Fidia</b></p> <ol style="list-style-type: none"> <li>1) Vitabu vya majedwali viwasilishwe kwa mlipa fidia nakala mbili (2) na nakala moja (1) kwenye ofisi za Mthamini Mkuu, Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa na Mthamini Kiongozi.</li> <li>2) Atakayehusika na gharama za fidia hiyo ni kijiji, mamlaka, kampuni, shirika, chama au Wizara inayohusika na uchukuaaji wa ardhi hiyo kwa ajili ya shughuli zake.</li> <li>3) Malipo yafanywe na wahasibu wa mlipa fidia au kupitia Mamlaka ya Serikali iliyoruhusu kuchukuliwa kwa eneo husika kama vile Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Halmshauri au pia Wizara ya Ardhi kwa miradi mikubwa ya Kitaifa.</li> <li>4) Fidia italipwa tu kwa nyumba iliyojengwa na mazao yaliyopandwa <b>kabla</b> sehemu ya ardhi inayohusika haijachukuliwa kwa matumizi ya shughuli nyingine.</li> <li>5) Aidha, sehemu inayohusika isifanyiwe shughuli mpya kabla fidia haijalipwa.</li> <li>6) Malipo yashuhudiwe na viongozi wa mitaa ya wananchi husika na mthamini aliyeshiriki zoezi.</li> <li>7) Mfidia aje na picha (passport size), vitambulisho na vithibitisho vinavyokubalika kijamii/kitaifa</li> <li>8) Michanganuo ya mali kwa kila mfidiwa iambatanishwe wakati wa malipo.</li> <li>9) Mfidiwa asainishwe kwenye jedwali la malipo; saina yake ya maandishi na dole gumba au mojawapo inapobidi.</li> <li>10) Kabla ya kupatiwa malipo, Mfidiwa asaini fomu ya kukiri malipo (disclaimant form).</li> </ol>	
<p><b>11.0 THAMINI ZA FIDIA ZENYE MALIPO YA ZIADA</b></p>	
<p>Taasisi za kimataifa na hasa zile zilizoko chini ya Benki ya Dunia na Umoja wa Mataifa, zimekuwa na utaratibu wa kutoa miogozo yenye malipo ya ziada kwa wananchi wanaondolewa kwenye maeneo inakotekelezwa miradi yao. Ni muhimu Wathamini wakatambua kuwa uthamini wa fidia ni</p>	

<p>wa kisheria ambao unaongozwa na sheria mahsusi.</p> <p>Hivyo, inapotokea Mthamini analazimika kuingiza malipo hayo kwenye taarifa yake, anatakiwa kufanya yafuatayo:-</p> <ol style="list-style-type: none"> <li>1) kupata waraka wa Taasisi husika unaotoa maelekezo ya malipo hayo.</li> <li>2) Kuambatanisha orodha ya malipo ya ziada na kuyaweka kama kiambatanisho kwenye taarifa ya Uthamini.</li> <li>3) Kimsingi, malipo ya ziada ya fidia kwa kuzingatia matakwa ya miongozo nje ya sheria za nchi yatahesabika kama maamuzi ya taratibu za kiutwala na siyo kwa mujibu wa sheria na taaluma ya uthamini.</li> <li>4) Hivyo, wathamini wanatakiwa kujiepusha na kuchanganganya malipo ya kisheria na yasiyo ya kisheria kwa kuwa yatakayoidhinishwa na Mthamini Mkuu ni yale tu yaliyozingatia matakwa ya sheria zetu taaluma.</li> </ol> <p>Aidha, endapo mlipa fidia ataenda kulipa fidia ya ziada, atafanya hivyo bila kuathiri kazi ya taaluma kwa namna yoyote ile. Kiongezwe kiwango mlingano (flat rate) kwa walipwa fidia wote bila ya kuwa sehemu ya Hati ya fidia iliyoandaliwa kitaalam na kisheria</p>	
<p><b>12.0 VYANZO MALALAMIKO YA FIDIA NA USHUGHULIKIAJI</b></p>	
